

SHULE YA SEKONDARI NGULU,
S. L.P 76, SIKONGE.
Barua Pepe;ngulusekondari@gmail.com
Mob.0787 113 616.

Tarehe 10/12/2019

Kumb, Na.NSS/FI/2020/.....

Jina la Mwanafunzi.....

S.L.P 127,

MBIRANI –SIKONGE.

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGULU, WILAYA YA SIKONGE, MKOA
WA TABORA MWAKA 2020**

1.0 Utangulizi.

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020 Shule ya Sekondari Ngulu ipo umbali wa Km 1 Kaskazini Mashariki mwa Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 06/01/2020 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 02/01/2020 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 07/01/2020 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo ya muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule;Soma kiambatanisho A

2.2 Daftari,kalamu na-mkebe.

2.1 Sheria na Kanuni muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya mwaka 1995.Aidha,Inazingatia Miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi yenye dhamana na Elimu Nchini na Ofisi ya Raisi –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,Wafanyakazi wote,Wanafunzi wengine,na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalioya jioni (Preparation) ni lazima.
- d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa ni lazima.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifumaelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika Shule hii.
- f) Kutunza usafi wa Mwili,Mavazi na Mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare kamili za Shule Kikamilifu Wakati wote unapotakiwa ndani na nje ya Shule.
- h) Kuzingatia ratiba yua Shule wakati wote na
- i) Kutunza mali za Umma.


3.2 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au kusimamishwa Shule

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- h) Kuwa mjamzito /kupata mimba.
- h) Kuoia au kuolewa.
- i) Kutoa mimba.
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- a) Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekolaza kikamilifu.


MKUU WA SHULE